



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA  
(Barua zote zitumwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi)



**MKOA WA MTWARA**  
Simu Na. 023 2410030  
Nukushi. 023 2410030  
Baruapepe: [ded@tandahimbadc.go.tz](mailto:ded@tandahimbadc.go.tz)  
Tovuti: [www.tandahimbadc.go.tz](http://www.tandahimbadc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P. 03,  
**TANDAHIMBA.**

Kumb Na. LA.121/228/02/74

22/09/2024

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba anawatangazia watumishi wote wa Umma wa Tandahimba nafasi ya kazi za muda kwa ajili ya shughuli za uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Tarehe 27, Novemba, 2024

**1.0 NAFASI**

I. Mwandikishaji wa wapiga kura (Nafasi 650)

**2.0 SIFA ZA MWOMBAJI.**

- Awe raia wa Tanzania
- Mwombaji lazima awe Mtumishi wa Umma
- Awe mwadilifu
- Asiwe kiongozi wa Chama cha Siasa
- Awe mkazi wa Halmashauri ya Tandahimba
- Awe na elimu angalau kidato cha nne
- Mwombaji aambatanishe vyeti vya taaluma na picha moja ya rangi ya hivi karibuni (Pasport size)
- Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV)
- Barua ipitishwe na msimamizi wa mtumishi katika kituo chake cha kazi
- Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
- Watendaji wa kata na vijiji hawaruhusiwi kuomba nafasi hii
- Mwisho wa Kupokea Maombi ni tarehe 27/09/2024 saa 9:30 Alasiri.

### 3.0 JINSI YA KUOMBA

Barua ya Maombi iandikwe kwa Mkono, ikiwa na majina kamili, kazi ya mwombaji, nafasi anayoomba, namba ya simu na kituo cha kazi.

zitimwe kwa;

Msimamizi wa Uchaguzi

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba

S.L.P 03

Tandahimba.

DCI. Mariam S. Mwanzalima  
Msimamizi wa Uchaguzi (W)  
**TANDAHIMBA**



**Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa**



*Kauli mbiu: Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze kushiriki Uchaguzi.*